**14B-Nuwn Saakinah Na Tanwiyn -Al-idghaam – Kuingiza, Kuchanganya.**

**ii- الإِدْغاَم Al-idghaam – Kuingiza, Kuchanganya.**

Idghaam ni kuingiza kitu kwenye kitu.

Katika hukmu za Tajwiyd ni kuingiza herufi saakin kwenye herufi yenye *i'raab* na kuzipelekea herufi mbili hizi kuwa herufi moja ya pili nzito. Na hutokea pale nuwn saakinah au tanwiyn inapofuatiwa na moja ya herufi sita za idghaam ي ر م ل ن و ambazo zinakusanyika katika ibara ya **يَرْمُلُون**

**Sharti ya Idghaam:**

Idghaam haiwezekani ikawa katika neno moja bali ni lazima nuwn saakinah au tanwiyn iweko mwisho wa neno la kwanza, na herufi inayoingizwa hiyo nuwn saakinah au tanwiyn مُدْغَماً فِيهِ (*mudghaman-fiyhi*) iweko mwanzo wa neno linalofuatia.

Ama inapokuweko nuwn saakinah katika neno moja na kufuatiliwa na herufi yoyote katika herufi za idghaam, hukmu ya idghaam hutoweka na kinachotakikana ni idhwhaar (kuidhihirisha nuwn saakinah); na hii inaitwa **إظهار مُطْلَقْ** (Idhwhaar Mutwlaq - Idhwhaar halisi.) Na katika Qur-aan kuna maneno manne tu ambayo nuwn saakinah iliyoko katika neno moja, imekutana na herufi mbili miongoni mwa herufi za idghaam. Herufi zenyewe ni و ي . Hivyo ni wajibu kuidhihirisha nuwn saakinah kwani kuleta idghaam pahala kama hapo ni kulibadilisha na kulipotosha neno na maana yake. [1]. Maneno manne hayo ni kama ifuatavyo:

---

[1] Sababu ya kuweko **إظهار مُطْلَقْ** ni kuhakikisha kwamba maana ya neno haibadiliki, kwani itakapoletwa hukmu ya idghaam itabadilisha maana na pia itasomeka ifuatavyo na kutokufahamika:

**دُياًّ قِوَّانٌ صِوَّانٌ بُيَّانٌ**

| Suwrah/ Aayah | Aayah | Neno |
|---|---|---|
| Al-'Imraan (3: 185) | وَمَا ٱلۡحَيَوٰةُ ٱلدُّنۡيَآ إِلَّا مَتَٰعُ ٱلۡغُرُورِ | ٱلدُّنۡيَآ [2] |
| Al-An'aam (6 :99) | وَمِنَ ٱلنَّخۡلِ مِن طَلۡعِهَا قِنۡوَانٞ دَانِيَةٞ | قِنۡوَانٞ [3] |
| Ar-Ra'd (13 : 4) | وَفِي ٱلۡأَرۡضِ قِطَعٞ مُّتَجَٰوِرَٰتٞ وَجَنَّٰتٞ مِّنۡ أَعۡنَٰبٖ وَزَرۡعٞ وَنَخِيلٞ صِنۡوَانٞ وَغَيۡرُ صِنۡوَانٖ يُسۡقَىٰ بِمَآءٖ وَٰحِدٖ وَنُفَضِّلُ بَعۡضَهَا عَلَىٰ بَعۡضٖ فِي ٱلۡأُكُلِۚ إِنَّ فِي ذَٰلِكَ لَأٓيَٰتٖ لِّقَوۡمٖ يَعۡقِلُونَ ٤ | صِنۡوَانٞ صِنۡوَانٖ [4] |
| As-Swaff (61 : 4) | يُقَٰتِلُونَ فِي سَبِيلِهِۦ صَفّٗا كَأَنَّهُم بُنۡيَٰنٞ مَّرۡصُوصٞ | بُنۡيَٰنٞ [5] |

**Tanbihi:**

Katika kuzisoma Aayah mbili za mwanzo za Suwrat Yaasiyn na Suwratul-Qalam, pale mtu anapopenda kuziunganisha Aayah hizo mbili, haipasi

[2]Imekariri mara nyingi katika Qur-aan
[3]Pekee katika Qur-aan
[4]Imekariri mara mbili katika Qur-aan kwenye Aayah hiyo moja.
[5]Imekariri pia: (At-Tawbah 9: 109, 110), (An-Nahl 16: 26), (Al-Kahf 18: 21), (Asw-Swaffaat 37: 97)

kuzipa hukmu ya idghaam japokuwa ن zinazotamkwa kwa sukuwn zinafuatiliwa na herufi ya و ambayo ni miongoni mwa herufi za idghaam, kwa sababu kutokana na Hafsw 'An 'Aaswim *twariyq Shatwabiyyah* inakuwa ni waajib kuifanya idhwhaar:

يسٓ ۝١ وَٱلۡقُرۡءَانِ ٱلۡحَكِيمِ ۝٢ [6]

Isomwe: يَاسِـــينْ وَالْـقُـرْآنِ الْحَـكِـيم ***((Yaasiyn wal-Qur-aanil-Hakiym)*** kwa kuidhihirisha ن katika يَاسِينْ bila ya ghunnah.

نٓ ۚ وَٱلۡقَلَمِ وَمَا يَسۡطُرُونَ ۝١ [7]

Isomwe: نُونْ والْقَلَمِ وَمَا يَسْـطُرُونْ ***((Nuwn wal-qalami wa maa yastwuruwn))*** wa kuidhihirisha ن katika نُونْ bila ya ghunnah.

Aina za idghaam ni kama ifuatavyo:

- **إِدْغَامُ بِغُنَّة Idghaamu bighunnah**

  Idghaam bighunnah ni kuingiza nuwn saakinah au tanwiyn kwenye herufi za ي ن م و pamoja na kuleta ghunnah inayotokea puani. Hukmu hii hutokea pale nuwn saakinah au tanwiyn inapofuatiwa na moja ya herufi hizo nne za idghaam bighunnaah nazo zimekusanywa katika ibara ya: **يَنْمُو** .

[6]Yaasiyn (36 : 1-2)
[7]Al-Qalam (68 : 1-2)

Mifano Ya إِدْغَامُ بِغُنَّة -Idghaamu bighunnah

| Tanwiyn | | Nuwn saakinah | | Herufi |
|---|---|---|---|---|
| Inavyotamkwa | Mfano | Inavyotamkwa | Mfano | |
| wujuwhuy-yawmaidhin | وُجُوهٌ يَوْمَئِذٍ | iy-yaquwluwna | إِن يَقُولُونَ | ي |
| yawmaidhiy-yuwaffiyhimu | يَوْمَئِذٍ يُوَفِّيهِمُ | wa may-ya'mal | وَمَن يَعْمَلْ | |
| rizqannahnu | رِزْقًا نَّحْنُ | wa mannu-ámmirhu | وَمَن نُّعَمِّرْهُ | ن |
| malikannuqaatil | مَلِكًا نُّقَاتِلْ | minni'matin | مِّن نِّعْمَةٍ | |
| swiraatwammustaqiymaa | صِرَاطًا مُّسْتَقِيمًا | mimmaaaaain | مِّن مَّآءٍ | م |
| maaimmahiyn | مَّآءٍ مَّهِينٍ | mimmasad | مِّن مَّسَدٍ | |
| Rahiymuw-Waduwdu | رَحِيمٌ وَدُودٌ | miw-waaqin | مِن وَاقٍ | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **waliyyiw-walaa** | وَلِيٍّ وَلاَ | **miw-waliyyin** | مِن وَلِيٍّ | و |

- إِدْغَامُ بِغَيْرِ غُنَّة **Idghaamu bighayri ghunnah**

إِدْغَامُ بِغَيْرِ غُنَّة (Idghaamu bighayri ghunnah) ni kuitia na kuichanganya nuwn saakinah au tanwiyn katika herufi za ر ل bila ya kuleta ghunnah inayotokea puani.

Mifano ya إِدْغَامُ بِغَيْرِ غُنَّة (Idghaamu bighayri ghunnah)

| **Tanwiyn** | | **Nuwn saakinah** | | **Herufi** |
|---|---|---|---|---|
| **Inavyotamkwa** | **Mifano** | **Inavyotamkwa** | **Mifano** | |
| **la-RauwufuRrahiym** | لَرَءُوفٌ رَّحِيمٌ | **mirrabihim** | مِن رَّبِّهِمْ | ر |
| **thamaratirrizqan** | ثَمَرَةٍ رِّزْقًا | **mirrizqin** | مِن رِّزْقٍ | |
| **hudallimuttaqiyna** | هُدًى لِّلْمُتَّقِينَ | **walaakillaa** | وَلَكِن لاَّ | ل |
| **qasamullidhiy** | قَسَمٌ لِّذِى | **milladun** | مِن لَّدُنْ | |

Kisha katika aina mbili hizo za idghaam, zinagawanyika kwa kuwa ziko zilizo kamilifu; إدْغَام كامِل (Idghaamu kaamil) na zilizopunguka; إدْغَام نَاقِص (Idghaamu naaqisw)

**إدْغَام كامِل - Idghaamu Kaamil** (Iliyokamilika) ambayo inaweza kuwa ni bighunnah au bighayri ghunnah. Herufi zake ni nne nazo zimekusanyika katika neno نرمل .

**إِدْغَامُ كامِلٍ بِغُنَّة Idghaamu Kaamil Bighunnah**– Hukmu hii hutokea pale nuwn saakinah au tanwiyn inapokutana na herufi za ن na م ikaingia yote katika herufi ya pili bila kubakisha chochote katika nuwn ndio maana ikawa kaamil na hivyo basi husababisha shaddah. Ghunnah inayopatikana kutokana na hizi herufi mbili ni kwa ajili ya hizo ن na م *mushaddad* zina swiffah ya ghunnah ya asili.

**إِدْغَامُ كامِلٍ بِغَيْرِ غُنَّة Idghaamu Kaamil Bighayri Ghunnah :** Hukmu hii hutokea pale nuwn saakinah au tanwiyn inapokutana na herufi za ر ل na ikaingia yote katika herufi ya pili inayofuatia bila ya kubakisha chochote katika nuwn ndio maana ikawa kaamil na hivyo basi husababisha shaddah lakini hapa ghunnah haithibiti.

Alama za إدْغَام كامِل (Idghaamu Kaamil) katika nuwn saakinah ni kuondoshwa sukuwn katika nuwn na kuipa shaddah herufi inayofuatia. Alama ya إدْغَام كامِل (Idghaamu Kaamil) katika tanwiyn ni kufuatana *i'raab* mbili moja chini ya mwenziwe kwa upande kidogo na kuipa shaddah herufi inayofuatia[8]

---

[8] Alama hizi katika Msahafu ni vile tanwiyn zinavyokaa moja chini ya mwenziwe kwa upande kidogo na si katika usawa wa mstari mmoja kama ifautavyo:

خَيْرٌ لَّكُمْ غَفُورًا رَّحِيمًا بِفَٰحِشَةٍ مُّبَيِّنَةٍ عَذَابًا نُّكْرًا

Mifano ya إدْغَام كامِل Idghaamu Kaamil

**Tanbihi:** Zingatia rangi katika jedwali mbili zifuatazo za إدْغَام كامِل (Idghaamu kaamil) na إدْغَام نَاقِصْ (Idghaamu naaqisw) katika matamshi kwamba pale penye shaddah, herufi imekaririwa kutajwa katika herufi inayofuatia nuwn saakinah au tanwiyn bila ya kugawanywa, na kwamba pasipokuwa na shaddah herufi moja imebakishwa katika nuwn saakinah au tanwiyn na ya pili imetajwa katika herufi inayofuatia nuwn saakinah au tanwiyn.

| Inavyotamkwa | Tanwiyn | Inavyotamkwa | Nuwn Saakinah | |
|---|---|---|---|---|
| **yawmaidhi- nnaa'imah** | يَوْمَئِذٍ نَّاعِمَةٌ | **wamannu- 'ammirhu** | وَمَن نُّعَمِّرْهُ | ن |
| **yawmaidhi- mmusfirah** | يَوْمَئِذٍ مُّسْفِرَةٌ | **mimmaalin** | مِن مَّالٍ | م |
| **latadhkiratullil muttaqiyn** | لَتَذْكِرَةٌ لِّلْمُتَّقِينَ | **mallam yazid- hu** | مَن لَّمْ يَزِدْهُ | ل |
| **shaytwaanirrajiym** | شَيْطَانٍ رَّجِيمٍ | **mirrahmatihi** | مِّن رَّحْمَتِهِ | ر |

## إدْغَام نَاقِصْ **Idghaamu Naaqisw (Pungufu)**

---

Ni tofauti hali yake zinavyokuwa katika hukmu ya idhwhaar ambako zinapandiana moja juu ya mwenzake katika usawa wa mstari mmoja na si kwa upande kama ifuatavyo:

نَارًا حَامِيَةً    وَرَقَةٍ إِلَّا    كَرَّةٌ خَاسِرَةٌ

Ni pale nuwn saakinah au tanwiyn inapokutana na herufi za ي و na ikaingia katika herufi ya pili inayofuatia kwa kuibakisha swiffah ya nuwn saakinah au tanwiyn ambayo ni ghunnah na ndio maana ikaitwa naaqisw hivyo basi herufi ya pili yake haitiwi shaddah.

Alama ya إِدْغَـــام نَاقِـــصْ (idghaamu naaqisw) katika nuwn saakinah ni kuondoshwa sukuwn katika nuwn na herufi ya pili yake haina shaddah. Alama ya إِدْغَـام نَاقِصْ (Idghaamu naaqisw) katika tanwiyn ni kufuatiana *i'raab* mbili moja chini ya mwenzio kwa upande kidogo na kutoweka shaddah juu ya herufi inayofuatia kimaandishi. Ama kusoma ni lazima isomwe kwa shaddah.[9].

Mifano ya إِدْغَام نَاقِصْ (Idghaamu naaqisw):

| Inavyotamkwa | Tanwiyn | Inavyotamkwa | Nuwn saakinah | |
|---|---|---|---|---|
| tadhkirataw-wata'iyahaa<br><br>khaasiaw-wahuwa | تَذۡكِرَةً وَتَعِيَهَآ<br><br>خَاسِئًا وَهُوَ | maw-wujida ...<br><br>miw-waraqatin | مَن وُجِدَ<br><br>مِن وَرَقَةٍ | و |
| wayluy-yawmaidhin<br><br>ghishaawatuw-walahum | وَيۡلٌ يَوۡمَئِذٍ<br><br>غِشَٰوَةٌ وَلَهُمۡ | wamay-yattaqiLlaah<br><br>famay-ya-mal | وَمَن يَتَّقِ ٱللَّهَ<br><br>فَمَن يَعۡمَلۡ | ي |

Hitimisho la aina za Idghaam ni kama ifuatavyo:

إِدْغَامُ كامِلٍ بِغَيْرِ غُنَّة Idghaamu kaamilin bighayri ghunnah: herufi zake ni ر ل

إِدْغَامُ كامِلٍ بِغُنَّة Idghaamu kaamilin bighunnah: herufi zake ni م ن

إِدْغَامُ ناقِصٍ بِغُنَّة Idghaamu naaqiswin bighunnah herufi zake ni ي و

[9] Rejea tanbihi namba 146